

Maswali

1. Mbona Waisraeli walinun'gunika tena?
2. Nani aliamini Mungu?
3. Mungu aliambia Musa afanye nini?
4. Mbona Musa alikasirika?
5. Musa alifanya nini?
6. Nini ilitoka mwambani?
7. Mbona Musa hakufurahisha Mungu?
8. Mungu aliadhibu Musa namna gani?
9. Mungu alikuwa anatufundisha nini kwa hadithi hii?
10. Musa aliharibu hili somo namna gani?

Majibu

1. Waisraeli walikuwa na kiu. Hawakukuwa na maji.
2. Musa na Haruni waliamini Mungu.
3. Mungu alimwambia Musa achukue fimbo na azungumzie mwamba.
4. Musa alikasirika kwa sababu Waisraeli hawakuamini Mungu.
5. Musa alipiga mwamba mara mbili.
6. Maji yalitoka mwambani.
7. Musa hakutii amri za Mungu kamili.
8. Musa hakukubaliwa kuenda kwa Nchi ya Ahadi.
9. Mwamba ni thabiti na haubadiliki. Uwezo wa Yesu ni thabiti. Upendo wake haubadiliki. Mwamba ulipigwa ili upeane maji ya uzima. Yesu aliuwawa kupeana uzima wa milele.
10. Yesu alikufa mara moja. Musa alipiga mwamba mara mbili.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1



24 Musa apiga mwamba

Kwa Biblia Hesabu 20: 2—13


Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba lazima tutii amri za Mungu kamili

Somo

Waisraeli walienda kwa jangwa ya Sini. Lakini hakukuwa na maji. Bunde tu Waisraeli walikuwa na kiu. Walianza kunun'gunikia Musa na Haruni. Wakisema, "Mbona mmetuleta mpaka jangwani sisi wote. Tutakufia huku. Tulipokuwa Misri tulikuwa na matunda mengi ya kukula na maji ya kunywa. Kiu kitatuia hapa pahali pabaya."

Musa na Haruni waliamini Mungu. Walienda Maskani katikati ya kambi. Utukufu wa Mungu ulionekana kule. Mungu alizungumza na Musa, "Chukua fimbo yako na uzungumze na mwamba. Amrisha maji yatoke kwa mwamba. Halafu kutakuwa na maji mengi ya watu wote kunywa."



Maskani

Musa alichukua fimbo. Alisanya Waisraeli pamoja. Musa alikasirika kwa sababu Waisraeli hawakuamini Mungu tena. Musa alipasia Waisraeli sauti, “Sikieni enye waasi, lazima tumtokezee maji kwa mwamba huu?” Musa alikasirika sana, tena aliogopa. Aliona kwamba asipowapa watu maji, watampiga kwa mawe. Kwa hivyo Musa alipiga mwamba kuhakikisha kwamba maji yametoka.



Mara tu, Musa alipopiga mwamba, maji yalitoka. Maji yalitiririka kutoka mwambani. Watu walikunywa maji ya kuwatosha. Walifurahi tena.

Lakini Mungu hakufurahia Musa. Musa alisema, “Lazima Tumtokezee maji kutoka kwa mwamba huu.” Hakukuwa Musa ndiye aliwapa maji. Alikuwa Mungu. Musa hakupea Mungu utukufu kwa kuwapea maji.

Musa hakutii Mungu kamili. Mungu aliambia Musa AZUNGUMZE na mwamba. Musa hakuamini Mungu kabisa. Hakutii Mungu kamili. Musa ALIPIGA mwamba mara mbili badala ya kuizungumzia.

Mungu aliadhibu Musa kwa sababu hakutii amri za Mungu kamili. Mungu aliambia Musa hatamkubali aende kwa nchi ya ahadi. Huu ulikuwa uchungu kuu kwa Musa. Musa aliongoza Waisraeli kwa miaka arobaini, lakini sasa hakubaliwi kuingia kwa nchi ya ahadi.

Kabla Musa afe, Mungu alimkubali aone nchi kutoka kwa mlima mrefu. Lakini hakukubaliwa kwenda kwa nchi. Tunajua wakati Yesu atarudi hapa duniani, atamfufua Musa kutoka kwa wafu. Ataenda kwa nchi ya ahadi na kukaa kwa Ufalme wa Mungu hapa duniani. Lakini hakukubaliwa kuenda kwa nchi na Waisraeli kwa sababu hakutii amri za Mungu kamili.

Hadithi hii inatufundisha umaana wa kutii amri za Mungu kamili. Katika Agano la Kale Mungu anatumfundisha masomo mengi juu ya Yesu atakapo kuja. Mungu alikuwa anatumonyesha somo juu ya Yesu lakini Musa akaharibu hili somo kwa kupiga mwamba tena. Musa alikuwa amepiga mwamba huko Refidimu kuwapa watu maji wanywe. Wakati huu Mungu alimwambia azungumze na mwamba.

Mungu alikuwa anatumonyesha somo juu ya Yesu alipomwambia Musa atoe maji mwambani.

Maji kutoka kwa mwamba	Yesu
Mwamba ni thabiti , haubadiliki	Yesu ako kama mwamba. Uwezo wa Yesu ni thabiti . Upendo wake kwetu haubadiliki
Maji yanatuwezesha kuwa hai. Bila maji tunaweza kufa. Musa alipiga mwamba kuwapa watu maji ili wasikufe.	Yesu mwamba wetu, alizulubiwa kutupa tumaini ya uzima wa milele.

Yesu alikuwa afe mara moja. Musa aliharibu hili somo kwa kupiga mwamba mara mbili.